

Vital Records Office
280 State Dr,
Waterbury VT 05671-8370

Maelekezo ya Jumla

- Ombi lililojazwa na kutiwa sahihi **na** kitambulisho cha sasa vinahitajika ili kuomba nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa au kifo cha Vermont.
- Ili kuomba aina mbili za vyeti (kama vile cheti kimoja cha kuzaliwa na kimoja cha kifo), tumia nakala ya pili ya ombi kwa kila aina ya cheti.
- Omba vyeti vya watu tofauti kwa maombi tofauti.
- Nakala nyingi za cheti kimoja zinaweza kuombwa kwa ombi moja.
- Vipengee vilivyotiwa alama kwa kinyota (*) **lazima** vijazwe.

Cheti cha Kuzaliwa au Cheti cha Kifo

- Ingiza majina na tarehe kwa usahihi. Ikiwa taarifa iliyo katika ombi ina makosa, huenda tusiweze kupata rekodi.
- Pitia faharasa ya umma ya jimbo zima ili kuangalia tarehe ya tukio au taarifa nyingine:
<https://secure.vermont.gov/VSARA/vitalrecords/search-tool.php>
- Chini ya Jina la Wazazi tumia jina la mwisho la mzazi lililotumiwa kabla ya ndoa yake ya kwanza, linalojulikana kama jina la ukoo la kabla ya ndoa, ikiwa lipo.

Maelezo ya Mwombaji

- Vyeti vitatumwa kwa anwani ya barua ya mwombaji iliyoingizwa kwenye ombi.

Uhusiano na Mtu Aliyetajwa Kwenye Cheti

- Ni watu walio na mojawapo ya mahusiano yaliyoorodheshwa katika sehemu hii ya ombi pekee wanaostahiki kuomba nakala iliyothibitishwa ya cheti cha kuzaliwa au cha kifo kulingana na sheria ya Vermont (18 V.S.A. § 5016 (b) (2)).

Hati ya(za) Utambulisho

- **Hati moja (1) kuu ya sasa ambayo muda wake wa kutumika haujaisha** kutoka orodha iliyo kwenye ombi inahitajika. Ikiwa huna mojawapo ya vitambulisho hivi vilivyotolewa na serikali, **hati mbili (2) mbadala** kutoka orodha iliyo kwenye ombi zinahitajika.
- Anwani iliyo katika hati ya(za) utambulisho lazima ilingane na anwani ya barua ya mwombaji iliyo kwenye ombi.
- Ikiwa unatuma ombi kwa barua, jumuisha nakala za hati za utambulisho. Hakikisha kwamba nakala hizo zinaweza kusomwa.

Muhtasari wa Agizo

- Ada ya nakala iliyothibitishwa imewekwa na sheria ya Vermont (18 V.S.A. § 5017).
- Toa hundi au hawala yako ya fedha inayolipwa ilivyoagizwa kwenye ombi.
- Tuma kwa barua au ulete malipo, ombi na hati za utambulisho kwenye eneo lililobainishwa kwenye ombi.

Uthibitishaji

- Baada ya kupitia maelezo yaliyo kwenye ombi lililojazwa, chapisha ombi hilo (ikiwa unajaza toleo la kielektroniki) na kisha utie sahihi na kuandika jina lako na uongeze tarehe.